East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature
*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya
Volume-9 | Issue-3 | Mar- 2026 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2026.v09i03.005

OPEN ACCESS

**Original Research Article**

# Ubainishaji wa Vipengele vya Ujumi wa Kiafrika na Athari yake katika Ushairi wa Kiswahili: Uchunguzi wa Ushairi wa Bongo Fleva

Costansia Urassa[1*]
[1]Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

**Article History**
**Received:** 10.01.2026
**Accepted:** 05.03.2026
**Published:** 16.03.2026

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Makala haya yalichunguza ujitokezaji wa ujumi wa Kiafrika katika ushairi wa Kiswahili wa Bongo Fleva pamoja na athari yake katika ushairi huo. Tafiti kuhusu vipengele vya ujumi wa Kiafrika zimeishia katika kubainisha ujitokezaji wake pasi na kuonesha athari (matokeo) yake katika kazi husika. Hali hii inachangia kutobaini umuhimu wa ujumi huo katika kazi za kifasihi za jamii ya Kiafrika jambo linalochangia baadhi ya kazi za kifasihi kutokusawiriwa vyema katika jamii. Data za makala haya zilipatikana katika maktaba ya kidijiti kwa kutazama na kusikiliza mashairi ya Bongo Fleva kisha kuchambua ujitokezaji wa ujumi wa Kiafrika na athari yake katika ushairi huo. Njia hii ilitumika kwa sababu njia nyingine za ukusanyaji wa data zisingeweza kuzifikia data zinazopatikana katika maktaba ya mtandaoni. Uchambuzi wa data za makala hii uliongozwa na Nadharia ya Ujumi Mweusi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa, ujumi wa Kiafrika katika ushairi wa Bongo Fleva una athari kubwa katika ushairi huo. Athari hiyo imebainika kusababishwa na usawiri kwa mawanda mapana vipengele vya Ujumi wa jamii wa Kiafrika ambavyo ni umoja na ushirikiano, ushababi, matumizi ya lugha za Kiafrika katika kukuza ama kubomoa kazi ya kifasihi, matumizi ya mazingira halisi ya jamii za Kiafrika pamoja na kipengele cha utu na ukarimu. Vipengele hivyo vimekuwa na athari (matokeo) kama vile kujenga diplomasia ya kisanaa baina ya mataifa ya Kiafrika, kuibua utalii wa ndani na nje ya Tanzania, kujenga umoja wa kisanaa baina ya wasanii ndani na nje ya Tanzania pamoja na kuleta umajumui wa kibara katika sanaa. Kwa muktadha huo, wasanii wanashauriwa kuendelea kutunga nyimbo zenye kusawiri ujumi wa Kiafrika kwa mawanda mapana. Hali hii itasaidia kazi za kifasihi za jamii mahususi (ikiwemo ushairi wa Bongo Fleva) kupata ukubalifu katika jamii kwa urahisi kuliko ingekuwa vinginevyo.

**Keywords:** Istilahi Muhimu: Ujumi, Ujumi wa Kiafrika, Ushairi wa Bongo Fleva, Athari.

**Copyright © 2026 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI NA MAPITIO

Ujumi wa jamii ni miongoni mwa mambo yanayoweza kufanya kazi ya fasihi ya jamii fulani kukua ama kupotea katika jamii (Davies na wenzake, 2009). Ujumi wa Kiafrika una nafasi kubwa katika kukuza ama kufifisha kazi za fasihi katika jamii ya Kiafrika. Hii ni kutokana na hoja kwamba, kazi yoyote ya kisanaa hufungamana na ujumi wa jamii yake (Senyamanza, 2011), na ujumi hujishughulisha na kutathmini uzuri au ubora wa sanaa, na kwa upande mwingine ubaya na udhalili wa sanaa hiyo (Barret, 2002). Licha ya umuhimu huo, tafiti mbalimbali zimekuwa zikichunguza zaidi ujitokezaji wa ujumi wa Kiafrika katika kazi za fasihi hasa katika kipengele cha maudhui na kusahau kuzungumzia athari yake katika kazi za jamii mahususi. Jambo hili linachangia kushindwa kuupa ujumi nafasi sahihi katika kazi za sanaa za jamii hizo. Sambamba na hayo, baadhi ya kazi za kisanaa za jamii mahususi zinashindwa kusawiriwa vyema katika jamii zao ingawa zinajinasibisha na ujumi wa jamii husika.

Mathalani, kumekuwepo na mtanziko wa kimtazamo na kiuchambuzi kuhusu ukubalifu wa ushairi wa Bongo Fleva katika jamii ya Kiafrika. Wengine huuona kwa mtazamo kwamba unavunja ujumi na utamaduni hivyo haukubaliki (Chachage, 2002; Suriano, 2006, 2007; Mwanjoka, 2011). Kutokana na hali hiyo ingeweza kufanya sanaa hiyo kukumbwa na kadhia ya mtenguo. Jambo lisilotarajiwa ni kwamba ni sanaa inayokua, inayostawi na kuongeza wigo kimawanda ndani na nje ya Tanzania (Avidan, 2023: Kasiga, 2023). Pia, zipo tafiti zinazoonesha kukubalika kwa ushairi huu

***Corresponding Author:** Costansia Urassa
Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

katika jamii (Omari, 2009; Sanga, 2011; Samwel, 2012; Avidan, 2023). Tafiti hizi zinarejelea kuwa Bongo Fleva ni sanaa yenye maudhui ya kizazi kipya (yaani kizazi cha sasa). Hali ya mtanziko huo inatia msukumo na hamasa ya kuchunguza ujumi wa Kiafrika katika ushairi wa Bongo Fleva na nafasi yake katika maendeleo ya ushairi huo.

**2.0 Dhana ya Ujumi**

Wanazuoni mbalimbali wanaeleza kwamba, ujumi ni dhana inayotokana na neno la Kiingereza *Aesthetics* lililotokana na neno la Kigiriki *Ais-thelikos* likiwa na maana ya hisia za akili (Armstrong, 1879; Bowman, 1998; Barret, 2002). Ujumi ulitazamwa kwa mwelekeo wa kifalsafa na kabla ya karne ya 17 neno ujumi halikuwa linatumika. Chimbuko lake lilitokana na mawazo ya Alexander Guttlieb (1735) miongoni mwa wanafalsafa wa Kijerumani ambaye kwa mara ya kwanza katika karne ya 18 aliunganisha vipengele vya ‘mguso’ na ‘hisia’ na kuibuka na neno ujumi (Fannon, 1952). Kuanzia nyakati hizo dhana hiyo ilikuwa ikitumika katika falsafa kama sayansi inayoshughulikia udhibiti wa utambuzi kwa hisi (Lopes, 2015). Hivyo, dhana ya ujumi ilitoka katika Nadharia ya Hisia za Akili na iliitwa falsafa ya ujumi ama falsafa ya sanaa. Katika mtazamo kama huo, Kant (1970) anabainisha kwamba suala la ufahamu kwa njia ya hisia ndilo linaloamua ujumi na uzuri ni jambo la kiulimwengu na huweza kupambanuliwa kama vitu kuwa kizuri ama si kizuri kutokana na vionjo vya mhusika katika kazi ya sanaa. Kufikia karne ya 20 tafiti kuhusu ujumi zimeweza kutumika katika nyanja mbalimbali kama vile falsafa, saikolojia, sosholojia na sanaa (Barret, 2002) na kila nyanja zimefasili ujumi kulingana na uwanja husika. Katika uwanja wa sanaa (fasihi ikiwemo) huweza kufasiliwa kama sayansi ya uzuri wa kazi ya sanaa. Ujumi wa kisanaa katika fasihi huonesha uzuri, ubaya ama uchanya na uhasi pamoja na elimu na sheria na kanuni za sanaa (Bosanquet, 1966).

**2.1 Ujumi wa Kiafrika katika Sanaa**

Kimsingi, kila jamii ina ujumi wake ambao huweza kutofautiana. Jamii ya Kiafrika kama zilivyo jamii nyingine duniani zina ujumi wake mahususi ambao hujulikana kama Ujumi wa Kiafrika ama Ujumi Mweusi (Zirimu, 1971). Wamagharibi walikuwa na mtazamo hasi kuhusu ujumi na sanaa za Kiafrika (Hume, 1975; Wolfgan, 1973). Hivyo, kuibuka kwa ujumi wa Kiafrika katika sanaa ni mojawapo ya jitihada za Mwafrika ulimwengu kuhusu ujumi na sanaa zake (Zirimu, 1971). Miongoni mwa njia zilizotumika ni watunzi wa Kiafrika kuonesha ujumi wao katika sanaa zao. Dorsey (1973) anabainisha kwamba tofauti kubwa kati ya sanaa ya Kiafrika na sanaa ya Kimagharibi ni matumizi yake. Sanaa ya Kiafrika imejinasibisha katika hali na miktadha ya maisha ya kila siku. Hivyo, sanaa ya Kiafrika iko sambamba na ujumi wake.

Fasihi Andishi ina tanzu kuu tatu ambazo ni riwaya, tamthiliya na ushairi (Mulokozi, 2017). Mbali na tanzu nyingine, utanzu wa ushairi una vipera na tanzu nyingine ndani yake. Miongoni mwazo ni ushairi wa Bongo Fleva unaotambulika kama ushairi wenye vionjo na ladha za Kitanzania wenye mseto na mitindo ya muziki wa vijana hasa katika jiji la Dar es Salaam, ukiwa na mchanganyiko wa muziki wa taratibu, muziki wa kufokafafoka, muziki wa haraka na midundo ya asili kama taarabu na dansi (Samwel, 2012; Avidan, 2023; Kasiga, 2023). Ushairi huu ulianza hapa Afrika Mashariki na kushika kasi miaka ya 1990 na 2000 kwa vijana wengi kujiunga na aina hii ya muziki. Kuna mtazamo kwamba ushairi huu haukubaliki miongoni mwa wanaharakati wa kimaadili, kidini, kijamii na kitamaduni. Miongoni mwa mambo yanayosababisha hayo ni uvunjifu wa ujumi na utamaduni. Isivyotarajiwa, ni sanaa inayokuwa na kuongeza wigo kimawanda. Kutokana na sababu hiyo tulipata msukumo wa kuchunguza vipengele vya ujumi wa Kiafrika katika utanzu huu ili kuweza kubaini mchango wake katika maendeleo ya ushairi huo.

Makala haya yalitumia data za maktaba ya kidijiti ambapo nyimbo sita (6) za Bongo Fleva zilitafitiwa. Uteuzi wa aina hii ya ushairi imetokana na sifa ya utanzu wenyewe yaani kukua, kuongeza mawanda ya kieneo kwa kasi kubwa licha ya kukataliwa na makundi mbalimbali katika jamii (Avidan, 2023; Kasiga, 2023). Kwa upande wa upatikanaji wa mashairi hayo, mtafiti alitumia vyanzo mbalimbali kama vile mitandao ya kijamii (*You Tube*, *Instagram*) na majukwaa binafsi ya wasanii. Usampulishaji nasibu tabakishi ulitumika kupata nyimbo sita (6) zilizotumika katika makala haya. Aina hii ya usampulishaji ilifaa zaidi kutumika kuteua kundi katika wango lenye data zilizoko katika kundi kubwa (Ary, Jacobs, Soensen na Razavieh, 2010). Data zilikusanywa kwa njia ya utazamaji, usikilizaji na udurusu wa matini. Nyimbo zilizotumika ni *Ndani ya Mateso* (2003) wa Happiness Thadei (p.h.k [1]. Sister P) ft [2]. Focus na Thomas, *Mimi Mmasai* (2010) wa Abel Loshilaa (p.h.k Mr. Ebbo), *Chochea Kuni* (2014) wa Mrisho Mpoto ft Lameck Ditto (p.h.k. Ditto), *Komassava* (2023) wa msanii Nasibu Abdul (p.h.k. Diamond Platinumz) ft Jason Joel De (p.j.k. Jason Derulo), *Waah!* (2020) na *Achii* (2021) za msanii Nasibu Abdul (p.h.k Diamond Platinumz) ft Kofi Olomide kutoka Kongo. Ufafanuzi na uchambuzi wa data uliongozwa na mkabala wa kitaamuli.

**3.0 Historia Fupi ya Ushairi wa Bongo Fleva**

Ushairi wa Bongo Fleva una historia ndefu. Kwa mujibu wa Omari (2009), Mwanjoka (2011) na Samwel (2012), jina “Bongo Fleva” kietimolojia limeundwa na maneno mawili ya lugha mbili tofauti ambayo ni “Bongo” lugha ya Kiswahili na “Fleva” lugha

[1] p.h.k ina maana kwamba ‘pia hujulikana kama’

[2] ft- inamaanisha ameshirikisha msanii anayetajwa baada ya msimbo huo

ya Kiingereza '*Flavor*'. Neno 'Bongo' limetumika kama sitiari kumaanisha akili na Fleva (*Flavor)* humaanisha ladha. Asili ya neno 'bongo' ni ugumu wa maisha uliowashughulisha wakazi wa jiji la Dar es Salaam ambao ulijumuisha kukosekana kwa ajira, hali ngumu ya biashara, bidhaa muhimu katika maisha ya kila siku kuadimika na watu kuishi mazingira magumu. Hali hiyo iliwalazimu wakazi wa jiji hilo kutumia akili ili kujipatia riziki. Aidha Omari (2009), Ismail (2011) na Avidan, (2023) wanaeleza, kutokana na hayo ilibainika kwamba, ili kuweza kuishi Dar es Salaam na kujipatia mahitaji ya msingi kama chakula, malazi na mavazi ni lazima kutumia ubongo yaani akili. Kwa mtazamo huo, jiji la Dar es Salaam lilibatizwa "Jiji la Bongo". Hata hivyo, haikuishia kurejelea jiji la Dar es Salaam pekee bali kwa miaka ya hivi karibuni, imevuka mipaka na kurejelea nchi nzima ya Tanzania (Samwel, 2015; Avidan, 2023). Historia hii inasaidia katika kubaini kwamba, neno 'bongo fleva' lina chanzo chake kutoka jamii ya Tanzania na hivyo sanaa ya Bongo Fleva ina umahususi wa jamii ya Watanzania.

Ushairi wa Bongo Fleva ulianza hapa Afrika Mashariki na kushika kasi kuanzia miaka ya 1990 hadi 2000 hasa ukiwa kama mwigo au utokeaji wa *Hip hop* kutoka Marekani. Hayo yalianza katika sherehe za shule, maonesho ya mitaani na katika fukwe. Makundi mengi yaliibuka mashuleni yakaanza kuimba muziki huo. Hali hii ikawa chanzo cha kukua na kuenea kwa Bongo Fleva katika maeneo mengi jambo ambalo lilifanya vijana wengi kujiunga na aina hii ya muziki. Ni katika msingi huo, Samwel (2015) anafasili Ushairi wa Bongo Fleva kuwa ni ushairi wenye vionjo au ladha ya Kitanzania ambao umepata umaarufu mkubwa kwa vijana nchini Tanzania hasa katika jiji la Dar es Salaam ukiwa na mchanganyiko wa muziki wa taratibu (*R&B)*, muziki wa kufokafoka (*Hip hop)*, muziki wa haraka (*dancehall)* na midundo ya asili kama taarabu na dansi.

Maandiko ya wataalamu hawa kuhusu ushairi wa Bongo Fleva yamesaidia katika kutoa uelewa mpana juu ya dhana, usuli na historia ya ushairi teule. Aidha, maandiko hayo yanathibitisha kwamba ushairi wa Bongo Fleva una asili ya kazi za sanaa ya Kiafrika (Tanzania) kwa kuwa ni ushairi wenye vionjo vya ladha ya Kitanzania vyenye mchanganyiko wa midundo ya asili kama taarabu na dansi za asili. Hivyo yanatoa ithibati ya kuhakiki ushairi teule kwa kuhusisha na Ujumi wa Kiafrika kwa kuwa ni sanaa ya Kiafrika.

**4.0 Nadharia**

Makala haya yaliongozwa na misingi ya Nadharia ya Ujumi Mweusi. Uteuzi wa nadharia hiyo ulitokana na hoja kwamba, elementi na misingi ya nadharia hiyo zinaeleza masuala yanayohusu ujumi wa Kiafrika moja kwa moja. Nadharia hii chimbuko lake ni kuibuka kwa vuguvugu la unegritudi lililohusu mabadiliko ya kitamaduni lililotokea miaka ya 1930 Paris, Ufaransa. Kabla ya hapo, watu wa Ulaya walichukulia Waafrika kama jamii ya watu wasio na uwezo wa kuwa na ujumi na sanaa yao (Hume, 1711-1776; Kant, 19710; Wamitila, 2002).Walidhani kuwa jamii za Kiafrika hazina ujumi wowote. Kwa hiyo, Nadharia ya Ujumi Mweusi iliibuka kama jitihada za wanasanaa wa Kiafrika za kupinga udhalilishaji waliokuwa wakifanyiwa na wakoloni kwa kuonesha kama watu wasio na maendeleo, wajinga na sifa nyingine kama hizo (Wafula na Njogu, 2007). Mawazo hayo yalimshughulisha Zirimu (1971) akapendekeza Nadharia ya Ujumi Mweusi akieleza, ujumi ni vigezo vya kuainisha urembo wa sanaa na vigezo hivyo hutokana na hali halisi iliyopo katika jamii husika. Kwa ujumla tunaweza kusema kuwa, ujumi Mweusi ni jumla ya mambo yanayojenga ustaarabu na taswira chanya ya ulimwengu wa Kiafrika. Kwa muktadha huo yapo mambo mengi yanayoweza kutumika katika kuchambua ujumi Mweusi katika kazi ya kifasihi hususani mashairi ya Kiswahili ya Bongo Fleva na kuweza kutoa picha dhahiri ya hayo yanayojadiliwa katika kazi hiyo na katika jamii husika. Katika uga wa sanaa nadharia hii iliendelezwa na Ojo-Ade (2004) akieleza kwamba ujumi Mweusi hasa kuanzia karne ya 20 unatumika katika kazi ya sanaa kuhakiki vitu, watu, mila na desturi zinazounda na kuendeleza dunia ya Mwafrika bila kuhusisha na maisha ya nje ya Afrika. Misingi ya nadharia hii imeshirikiana kwa pamoja katika kubainisha ujitokezaji wa ujumi wa Kiafrika katika mashairi ya Bongo Fleva pamoja na athari yake katika maendeleo ya ushairi huo.

## 5.0 MATOKEO YA UTAFITI

Kwa kutumia data kutoka maktabani kwa njia ya udurusu makini wa matini teule, makala haya yalifanikiwa kubainisha vipengele vya ujumi wa Kiafrika katika nyimbo teule. Vipengele hivyo ni vile vinavyoonekana kujitokeza katika ushairi teule na ambavyo vinasaidia ushairi huo kwenda sambamba na ujumi wa Kiafrika. Ujumi wa jamii unapojitokeza katika kazi ya kisanaa husaidia kudhihirisha kuwa kazi hiyo inajinasibisha na ujumi wa jamii hiyo hali ambayo inaweza kuifanya kazi hiyo kukubalika zaidi katika jamii husika (Renatus, 2018; Elihaki, 2023). Vipengele vilivyobainika vimejadiliwa kama ifuatavyo.

**5.1 Umoja na Ushirikiano**

Data zilizotafitiwa zimebaini kwamba, umoja na ushirikiano ni miongoni mwa kipengele cha ujumi wa Kiafrika kinachojenga sanaa ya Bongo Fleva kujinasibisha na ujumi huo. Kimsingi, utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika ulijengwa katika misingi ya umoja. Kabla ya mwingiliano wa wakoloni kuathiri utaratibu wa maisha ya Mwafrika, uzuri ulikuwa haupatikani nje ya maisha ya ushirika (Zirimu, 1971). Kwa hiyo, umoja na ushirikiano ni idili muhimu katika maisha ya jamii za Watanzania na Afrika kwa ujumla. Makala haya yamebaini kwamba, umoja na ushirikiano katika ushairi teule umejitokeza kwa namna ya wasanii wa Bongo Fleva kutoka Tanzania kufanya kolabo na kushirikiana na wasanii kutoka ndani na nje ya Tanzania katika sanaa ya muziki. Mathalani baadhi ya wasanii wa Bongo Fleva katika sampuli ya utafiti huu

waliowashirikisha wasanii kutoka nje ya Tanzania ni Nasibu Abdul (p.h.k. Diamond Platinumz) ameshirikiana na wasanii kadhaa kama vile msanii Kofi Olomide kutoka nchi ya Kongo katika nyimbo za *Waah*, *Achii!* , Jason kutoka Paris katika wimbo wa *Komasava* pamoja na wasanii wengine wengi. Hali hii imesaidia kujenga diplomasia ya kisanaa kwa baadhi ya mataifa ya Kiafrika. Diplomasia ni mchakato wa kuendeleza na kudumisha mahusiano mazuri kati ya mataifa na jamii mbalimbali ili kukuza ushirikiano na kudumisha amani kati ya pande hizo (mataifa hayo). Hivyo, uwezo wa wasanii kutoka Tanzania kufanya kolabo na wasanii mbalimbali kutoka mataifa mengine ya Afrika imejenga diplomasia baina ya Tanzania na mataifa walimotoka wasanii waloshirikishwa. Kwa hiyo, makala haya yamebaini kuwa katika Bongo Fleva, ujumi wa Kiafrika unaojitokeza katika umoja na ushirikiano haujitokezi tu katika maudhui kama tafiti nyingine zinavyobainisha (Omari, 2018; Sanga, 2018; Elihaki, 2023) bali pia hata kati ya wasanii, jamii na jamii ama taifa na taifa. Hali hii imesaidia katika kujenga diplomasia ya mataifa ya Kiafrika, na hii ndiyo athari yenyewe. Makala haya yameipa nafasi sifa hii katika ushairi teule jambo ambalo linawezesha sanaa hii kukua na kuongeza wigo wa kimawanda katika mataifa ya Kiafrika na nje ya Afrika ingawa haikubaliki kwa kiwangotarajiwa.

Vilevile, makala haya yamebaini ujitokezaji wa umoja na ushirikiano kwa njia ya kujenga umoja wa kisanaa. Nyimbo za Bongo Fleva zimesheheni vipengele vinavyosawiri hali ya umoja na ushirikiano hali ambayo inaonekana kuleta umoja wa kisanaa kati ya wasanii kwa wasanii, wasanii na hadhira na hata taifa na taifa. Mawazo ya kinadharia katika Nadharia ya Ujumi Mweusi yanaeleza kwamba, jinsi usawiri wa umoja na ushirika unavyosawiriwa katika kazi ya fasihi ndivyo inavyobainisha masuala ya ujumi wa Kiafrika yanavyojidhihirisha (Wafula na Njogu, 2007). Mashairi ya Bongo Fleva yaliyotafitiwa yanadhihirisha hayo pale yanapoonesha namna yalivyohusisha masuala ya umoja na ushirika. Umoja na ushirika kama sehemu ya ujumi wa Kiafrika imeelezwa katika tafiti mbalimbali zinazohusu ujumi wa Kiafrika kama vile Badru (2015), Laswai (2015) na Sanga (2023). Mathalani, Badru (2015) akitafiti kuhusu mabadiliko ya kiujumi anaeleza kuwa, falsafa ya ushirikiano inayojitokeza katika vitendawili vya Kiswahili inaonesha ushirikiano ndio nguzo ya kuimarisha mahusiano kuanzia ngazi ya kifamilia hadi ngazi ya kijamii. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya tafiti hizo. Lakini, tofauti na tafiti hizo, utafiti huu umebaini kwamba, umoja na ushirikiano katika nyimbo za Bongo Fleva unajitokeza kwa namna kadhaa. Kwa mfano, kuna umoja na ushirika wa wasanii. Data zilizotafitiwa imebainika kwamba, katika ushairi wa Bongo Fleva kumejitokeza ushirikiano baina ya wasanii ambao unajenga umoja wa kisanaa. Kama ambavyo imekwishaeleza katika aya zilizotangulia katika kipengele hiki kwamba, baadhi ya wasanii hufanya kolabo na wasanii wenzao kutoka ndani ama nje ya nchi (nchi nyingine za Kiafrika) katika kutunga ama kuimba mashairi. Hali hii inajenga umoja wa kisanaa baina ya wasanii hao. Ushirikiano huo hufanya wasanii kujiona wamoja na kufanya muziki wenye tija. Kwa hiyo, uzuri katika umoja na ushirikiano katika muziki wa Bongo Fleva unawafanya wasanii kutoka mataifa mengine kujiona wao ni sehemu ya Bongo Fleva.

Aidha, uzuri unaojitokeza katika ushirikiano baina ya wasanii ni kielezo cha kuchochea kuunganisha mchanganyiko wa tamaduni za muziki wa Tanzania na muziki wa mataifa walimotoka wasanii walioshirikishwa jambo ambalo linaleta muziki unaovuka mipaka ya kitamaduni. Hali hiyo imesaidia kwa kiwango kikubwa kufanya wasanii kujiona wamoja katika kuendeleza sanaa ya muziki Afrika. Mawazo hayo yanaungana na mawazo ya kinadharia ya Nadharia ya Ujumi Mweusi inayoeleza kuwa, kwa Waafrika mtu si mtu bila wengine (Taylor, 2010), kwa hiyo, katika muktadha huo umoja na ushirikiano unaleta ukamilifu wa sanaa. Pia, umoja na ushirikiano ni uzuri kwa kuwa unawezesha kufanikisha masuala mbalimbali katika jamii. Mashairi yaliyotafitiwa yanadhihirisha hayo kwa kiwango kikubwa, hali ambayo imesaidia kujenga diplomasia nzuri baina ya mataifa pamoja na kujenga umoja wa kisanaa miongoni mwa wasanii katika mataifa ya Kiafrika.

**5.2 Ushababi**

Ushababi ni sifa ya ujana inayoambatana na ushupavu, uhodari, nguvu katika kupigana na kufanya mambo ambayo si rahisi kufanywa na watu wengine (Zirimu na Gurr, 1973). Kwa mujibu wa Asante (1993), katika jamii za Kiafrika ushababi ni kipengele cha ujumi wa Kiafrika kinachohusisha hali ya vijana kwa na sifa ya ujasiri, uhodari na ushupavu. Kimsingi, katika jamii za Kiafrika ushababi ni kipengele muhimu katika kuchambua na kutazama uzuri wa Kiafrika. Hii ni kutokana na hoja kwamba uzuri ni sifa ya kikazi na kimatumizi (Asante, 1993). Utafiti uliozaa makala haya umebaini kuwa, sanaa ya Bongo Fleva imesheheni hali na matukio ya kishababi kwa kiasi kikubwa. Ni kipengele mojawapo kinachoonesha kuwa sanaa ya Bongo Fleva inakwenda sambamba na ujumi wa Kiafrika. Hii ni kwa sababu ushababi ni nguzo muhimu katika ujumi wa Kiafrika. Hali hii ni kutokana na hoja kwamba, baadhi ya washairi wa Bongo Fleva wana sifa za kishababi. Miongoni mwa sifa hii ni kuwa na ujasiri wa kupambanua sanaa ya Bongo Fleva kama sanaa ya Kiafrika kwa kuhusisha vipengele anuai vya ujumi wa Kiafrika katika sanaa hiyo hali inayosaidia kuunganisha Bara la Afrika kwa kutumia sanaa ya muziki. Ujasiri wa wasanii kutoka Tanzania wa kufanya sanaa na wasanii wakubwa kutoka nchi nyingine za Kiafrika kama vile Nigeria, Kongo, Kenya, Afrika ya Kusini umejenga ukubalifu wa sanaa ya Bongo Fleva ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya nyimbo alizoimba na wasanii kutoka nje ya Tanzania ni *Waah!* (2020) wa Diamond Platinumz ft Kofi Olomide kutoka Kongo, *Komasava* (2021) wa Diamond Platinumz ft Jason, *Make Me Sing* wa Diamond Platinumz ft A.K.A kutoka Afrika ya

Kusini kwa kutaja chache. Kwa mijibu wa makala haya, mtunzi wa nyimbo hizo anachukuliwa kama shababi wa Bongo Fleva kwa kuwa amekuwa na uthubutu wa kuivusha sanaa ya Bongo Fleva kutoka kuwa sanaa ya Tanzania na kuongeza wigo kimawanda na kustawi kwa kasi ukilinganisha na aina nyingine za sanaa.

Makala imebaini kwamba hali hiyo ni kutokana na jitihada binafsi za msanii kwa kuwa kitendo hicho kinatazamwa kama kitendo cha kishababi kwa kuwa wapo wasanii na sanaa ambazo hazikufanikiwa kufanya hayo ingawa walikuwa na fursa ya kufanya hivyo. Aidha, makala haya yamebaini pia kwamba, harakati za kujenga sanaa ya Bongo Fleva kwa kuhusisha vipengele vya ujumi wa Kiafrika kumeifanya sanaa hiyo kuonekana kuwa ni sanaa ya Kiafrika. Mawazo ya kinadharia ya Nadharia ya Ujumi Mweusi yamejenga hoja hii kwa kueleza kwamba, kwa kuhusisha ujumi wa Kiafrika katika sanaa kunamtambulisha Mwafrika na sanaa yake (Ojo- Ade, 2004). Lakini pia, Nadharia hii inaeleza, ujasiri wa kishababi huleta mafanikio yenye ushindi (Asante, 1993). Kwa muktadha huo, ushababi wa msanii Diamond Patinumz umeleta ushindi kwa kufanikiwa kutoa sanaa ya Bongo Fleva katika mipaka ya Tanzania na kuongeza wigo kimawanda ya nje ya Tanzania na Afrika kwa jumla. Makala yanaitazama hali hii kama ushindi mkubwa katika sanaa hiyo.

Sambamba na hayo, makala haya yamebaini kuwa, katika tasnia ya Bongo Fleva ushababi haujitokezi tu kwa mashabi kufanikiwa kuongeza wigo kimawanda, bali pia kuwa na ujasiri wa kutunga na kuimba kuhusu Uafrika wetu na kuonea fahari sanaa ya Kiafrika. Data zilizotafitiwa zimedhihirisha baadhi ya nyimbo za Bongo Fleva zenye kueleza kwa ujasiri kuhusu Afrika na kuonea fahari sanaa ya Kiafrika. Mathalani, katika wimbo *Mimi Mmasai* (2010) wa Abel Loshilaa (p.h.k Mr. Ebbo) kama inavyoonekana katika data namba 1, msanii anaimba.

Mimi Mmasai bhana, nasema Mimi Mmasai
Ni kitu najivunia Masai fahari yangu
Naruhusu kushangaa kwa wageni na wenyeji
Nadumisha mila, ile wengine imeshindwa
Tamaduni yenye nguvu iliyobaki Afrika

Katika data namba 1, tunaona msanii kwa ujasiri mkubwa anatambulisha ulimwengu kwamba jamii ya Kimasai ndio yenye utamaduni wenye nguvu kuliko tamaduni nyingine Afrika licha ya mwingiliano wa tamaduni ngeni katika jamii. Jamii hiyo bado inaenzi na kudumisha mila na desturi zao kwa kiwango kikubwa. Makala haya yanalitazama jambo hili kuwa ni la kishababi kwa kuwa wapo wasanii wengi ambao hawana ujasiri wa kueleza masuala yanayohusu jamii yao katika sanaa zao. Mtazamo huo unashabihiana na mtazamo wa kinadharia ya nadharia ya Ujumi Mweusi kwamba Waafrika wana tamaduni na desturi zao hazipaswi kukengeushwa (Zirimu, 1971). Hivyo, kazi za kisanaa hudhihirisha katika sanaa zao ili zitambulike na kuthaminiwa katika jamii.

Athari ya ujasiri wa kufanya sanaa na wasanii maarufu kutoka nje ya Tanzania inaweza kuivusha sanaa ya Bongo Fleva kutoka kuwa sanaa ya 'Bongo' na kuwa sanaa ya 'Afrika'. Lakini pia, ujasiri wa kuhusisha masuala ya Kiafrika katika ushairi teule imeiwezesha Bongo Fleva kueneza tamaduni za Kiafrika (ikiwemo lugha) huko ulimwenguni. Hali hiyo imeifanya sanaa ya Bongo Fleva kuendelea kuongeza wigo kimawanda ndani na nje ya Tanzania.

Mbali na ujasiri wa kutunga na kuimba kuhusu Uafrika na kuonea fahari sanaa ya Kiafrika, data za makala haya zimebaini pia kwamba, ushababi unaohusishwa na baadhi ya wasanii pamoja na mambo mengine, umesaidia kuibua masuala ya utalii wa ndani na nje ya Tanzania. Kwamba, katika nyimbo zaa Bongo Fleva hadhira inaweza kujifunza masuala ya utalii na kupata mazuri yanayopatikana katika taifa la Tanzania na kwingineko Afrika, na hii ndio athari yenyewe. Mathalani msanii Mr. Ebbo anadhihirisha haya katika wimbo wa *Mimi Mmasai* (2010) katika data namba 2 ubeti wa pili msanii anaimba.

Na ile Kinondoni, imegeuka kama Kongo
Kila kona Wakongo, wanaimba ndombolo
Wanapenda Masai, Yero sumbai nemeyolo
Hebu fundisha Mimi, kucheza kiwasense
Fundisha mimi kuruka juu

Katika data namba 2 msanii anajaribu kuijuza hadhira jinsi jamii ya watu kutoka nchi ya Kongo wameenea katika jiji la Dar es Salaam hasa maeneo ya Kinondoni kwa shughuli mbalimbali kama vile muziki na biashara. Hoja ya msingi hapo ni kuwa Wakongo wanapowaona Wamasai, kwanza wanawapenda kwa namna walivyo, mavazi yao na jinsi wanavyotumia lugha yao ya Kimasai mahala popote bila kujali kwamba kuna makabila mengine ambayo hayafahamu lugha ya kimasai. Kwa muktadha huo, mbali na kudhihirisha ushababi wa kueleza kuhusu jamii ya Kimasai, mtunzi anatueleza pia kuhusu utalii unaofanywa na jamii ya watu wa Kongo na jamii nyingine. Mtunzi anajaribu kuingia katika akili ya hadhira na kumshawishi kuielewa kuhusu jamii ya Kimasai. Ujasiri huo unachangia kupendwa kwa kiwango kikubwa katika jamii wanamoishi. Mtazamo unaoendana na maelezo hayo yaliwahi kuelezwa na Mandembwe (2011), Williady (2013), Sanga (2018) na Jim (2021) kuwa sifa ya kishababi hufanya mashababi kuwa na ujasiri wa kufanya mambo makubwa kwa kujiamini hali ambayo inawafanya mashababi hao kupendwa. Utafiti huu unakubaliana na mawazo ya tafiti zilizotagulia na umekwenda mbali zaidi na kuonesha namna ujasiri wa mashababi wa Bongo Fleva ulivyosaidia kuivusha sanaa ya Bongo Fleva kutoka hatua moja kwenda hatua ya mbele zaidi katika sanaa.

**5.3 Mazingira ya Kiafrika**

Kisingi, mazingira huweza kuwa mahali na wakati ambavyo hubainisha muktadha wa tukio,na

muktadha hutambulisha utamaduni wa jamii fulani. Aidha, mazingira huweza kuwa ni mahali halisi au mahali pa kufikirika (Madumulla, 2009). Kufahamu mazingira halisi katika kazi ya fasihi kunasaidia kuelewa hali ya maisha, hisia, imani, tabia na maumbile ya jamii husika (Njogu na Chimerah, 1999).Mazingira yaliyotazamwa katika makala haya ni mazingira halisi. Uhalisi katika nyimbo za Bongo Fleva zilizotafitiwa uliangaliwa kwa kuzingatia uwezo wa nyimbo hizo kusawiri mazingira asilia ya Kiafrika ambayo yaliwakilishwa na miji, vijiji, misitu, hali duni za maisha, uoto wake, mavazi, vyakula, vifaa mbalimbali vya Kiafrika kama vile mikeka, filimbi, majamvi, kuni nakadhalika, pamoja na mandhari nyingine za asili ambazo zinaonesha maisha halisi ya Waafrika. Sifa mojawapo ya ujumi Mweusi ni kuzungumzia mazingira asilia ya Kiafrika. Mazingira yanayosadifu Afrika katika kazi ya sanaa hujenga mahusiano ya kazi hiyo na mazingira ya jamii ya Kiafrika, na hii ni sifa muhimu ya ujumi wa Kiafrika (Ekwuru, 2000).

Makala haya yamebaini kuwa katika sanaa ya Bongo Fleva kuna matumizi makubwa ya mazingira asilia ya jamii ya Kiafrika hali inayojenga ujumi wa Kiafrika sambamba na sanaa hiyo. Data zilizotafitiwa zinathibitisha kwamba mashairi ya Bongo Fleva yanahusisha mazingira yanayosadifu uhalisia wa Kiafrika ni jambo linaloonesha uzuri wa sanaa hiyo katika uga wa Kiafrika. Kwa mfano katika wimbo *Chochea Kuni* (2014) wa Mrisho Mpoto ft Ditto, msanii anajaribu kuonesha hali halisi ya jamii ya Kiafrika huku akihusisha mazingira halisi ya Kiafrika yaliyobainishwa katika matumizi ya vifaa kama kuni, moto, mikeka kwa kutaja chache. Kwa mfano katika data namba 3 msanii anaimba,

Raha ya jamvi siku zote ni virakaviraka
Na mwacha asili siku zote ni mtumwa
Tawi kavu kuanguka wala si ajabu
Wakati wao wanatenganisha mavi ya panya kwenye unga
Ninyi chocheeni kuni zilizoloa ugali usongwe

Kadhalika matumizi ya mazingira asilia ya Kiafrika yamebainishwa katika wimbo *Mimi Mmasai* (2010) wa Mr. Ebbo, data namba 4 msanii anaimba.

Nimtume nani kule kwetu Longido
Aende samilia kule kwa mama Totoo
Maisha mbofu Bongo kila siku msoto
Sipati masiwa, nyama na ng'ombe mekosa
Nakula maharaki na ugali ngumu kumeza

Maelezo katika data namba 3 na namba 4 yanaonesha namna wasanii wanaeleza juu ya mazingira halisi katika jamii ya Kitanzania. Mathalani data namba 3 msanii anaeleza kuhusu mazingira yanayopatikana katika jamii ya Kimasai iliyopo mkoani Arusha pamoja na mkoa wa Dar es Salaam (Bongo) nchini Tanzania. Kupitia mazingira hayo imewezesha kufahamu hali ya maisha ya jamii ya Kimasai, shughuli za kiuchumi wanayojishughulisha nazo pamoja na namna ya kuthamini kile tulichonacho katika mazingira tunayoishi.Msanii anajaribu kueleza hadhira yake kwamba, mazingira ya Longido ni rafiki kwa shughuli za ufugaji wenye tija (kwa maana ya kupata nyama na maziwa) ukilinganisha na mazingira ya mkoa wa Dar es Salaam. Kwa hiyo, Bongo Fleva kutumia mazingira ya asili katika kunaruhusu kuonesha uzuri wa sanaa za Kiafrika. Mazingira ya Kiafrika ni ujumi wa Kiafrika ambao huonesha uzuri na thamani ya Uafrika katika sanaa za Kiafrika. Kazi mbalimbali za kifasihi zinazohusisha mazingira asili ya Kiafrika husaidia kazi hizo kujenga ukaribu kati yake na ujumi wa jamii ya Kiafrika.

**5.4 Matumizi ya Lugha za Kiafrika**

Matumizi ya lugha za Kiafrika katika muziki wa Bongo Fleva yanadhihirisha namna sanaa hiyo inavyotetea ujumi wa Kiafrika kwa kuwa lugha ni utambulisho wa jamii husika. Makala haya yamebaini kuwa, kuna matumizi ya lugha za Kiafrika katika sanaa ya Bongo Fleva kwa kiwango kikubwa yaliyojitokeza kwa namna mbili. Namna ya kwanza ni matumizi ya lugha za asili mchanganyiko (lugha zaidi ya moja) katika wimbo mmoja. Athari yake ni kuteka hadhira pana ya sanaa hiyo. Lakini pia ni ili kuweza kueneza lugha za Kiafrika katika mawanda mapana kiulimwengu. Vilevile, data za utafiti huu zinabainisha kuwa, matumizi ya lugha za Kiafrika zenye kusawiri vionjo mbalimbali vinavyosawiri ujumi mweusi yana mchango mkubwa katika kuonesha kwamba sanaa ya Bongo Fleva inakwenda sambamba na ujumi wa Kiafrika katika maendeleo yake. Lugha kama sehemu ya ujumi wa Kiafrika ina jukumu la kubeba na kuendeleza tamaduni za Kiafrika ndani na nje ya Waafrika wenyewe (Chirambo, 2006). Hali hiyo inachangia maendeleo ya ujumi katika jamii pana ya Waafrika na dunia kwa ujumla. Miongoni mwa nyimbo za utungo teule zinazotumia lugha za Kiafrika ni *Mimi ni Mmasai* (2010) wa Mr. Ebbo na *Waah* (2020) wa Diamond Patinumz ft Kofi Olomide. Mathalani katika wimbo wa *Waah* (2020) watunzi wametumia lugha mbili tofauti za Kiafrika (Kiswahili na Kilingala) kwa lengo la kuteka hadhira pana ya Afrika .Wimbo huu umeimbwa na wasanii wawili kutoka mataifa mawili tofauti huku kila mmoja akitumia lugha ya jamii yake. Katika data namba 5 msanii wa kwanza (Diamond) anaimba.

**Ondoa Na.4. 5, *Waah* (2020)**

Tamu kupendwa nawe
Taamu uuh, uuh
Ooh maneno maneno maneno tumeyazoea
Vijineno neno Tumeshazoea

Msanii wa pili (Kofi Olomide) katika ubeti huohuo anaimba kwa kutumia lugha ya Kilingala, data namba 6 msanii anaimba

| | |
|---|---|
| Oya Mose Kunambi jipepee | Tafsiri: Mose mwambie ajipepee |
| Oh Rcando Moma, Ee Jipepee | Ricado Moma (jina la mtu) |
| Nase Chubaka | Na pia Chubaka |

| | |
|---|---|
| Na se Joseph Berthier | Na pia Joseph Berthier (jina la mtu) |
| Na se Quadra alobi | Na pia Quadra alisema |

Lakini pia katika wimbo huo kuna wakati msanii kutoka Kongo anaimba kwa lugha ya Kiswahili. Data namba 7 msanii anaimba.
Yaani Dar salama Joto
Toa lesso jipepee
Oya Congo Joto
Toa lesso Jipepee
Jipepee jipepee ooh jipepee

Madondoo namba 5, namba. 6 na 7 yanaonesha matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kilingala (miongoni mwa lugha za Kiafrika) katika mashairi ya Bongo Fleva na ni namna mojawapo ya kuhusisha ujumi wa Kiafrika katika sanaa. Lugha ni miongoni mwa kipengele kinacholeta utambulisho wa Waafrika na utamaduni wao. Hisia mbalimbali zinazofungamana na utamaduni wa Kiafrika hudhihirika kupitia lugha. Jamii za Kiafrika hujiona zipo karibu zaidi na kazi zinazotumia lugha za Kiafrika zaidi kuliko kazi zinazotumia lugha za kigeni. Hii ni kwa sababu, kazi zilizoandikwa kwa lugha za Kiafrika zinakuwa na mawanda mapana ya usawiri wa vionjo mbalimbali vya utamaduni, mazingira na tajiriba kadha wa kadha katika jamii za Waafrika. Katika hili Chirambo (2006) anaeleza, mashairi yanayoimbwa kwa lugha ya jamii yake husawiri utamaduni wa jamii hiyo, na hubeba ujumbe unaoendana na utamaduni wa jamii hiyo. Mashairi ya Bongo Fleva yaliyotafitiwa yanatumia lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za jamii za Kiafrika. Lugha hizo zimejaa vionjo mbalimbali vinavyofungamana na utamaduni, mila na desturi za Waafrika. Hali hii inadhihirisha kwamba Afrika ina ujumi wake mahususi, ujumi huo husawiriwa kwenye kazi za fasihi ikiwemo mashairi ya Bongo Fleva.

Namna ya pili ni matumizi ya lugha yenye misemo, lugha za ishara, methali na mafumbo vinavyofungamana na muktadha na mazingira ya Kiafrika. Hali hii inajitokeza katika muziki wa Bongo Fleva na hasa kwa kurejelea mazingira na utamaduni wa Mtanzania kwa kiwango kikubwa. Hali hii inaleta ukaribu wa sanaa hiyo na hadhira yake. Kwa mujibu wa Yonazi (2019), lugha ni chombo kinachotumiwa na waandishi wa kazi ya fasihi kuibua hisia za kihalisia za jamii. Naye Renatus (2018) anaeleza kuwa, kadiri mwandishi anavyotumia lugha yenye vionjo ambavyo hugusa hadhira yake, ndivyo anavyofanikiwa kuteka hisia za hadhira na jamii kwa ujumla. Suala hili linaendana na mawazo ya Nadharia ya Ujumi Mweusi inayoeleza kuwa, kwa Waafrika lugha ni kipengele cha kiujumi chenye uzuri wa namna mbalimbali ambavyo ikitumika vizuri hujinasibisha na jamii husika katika kazi hiyo.

Aidha, data zilizotafitiwa zinaonesha ujitokezaji wa matumizi ya lugha za Kiafrika katika Bongo Fleva kama sehemu ya kuenzi na kuendeleza ujumi wa Kiafrika katika sanaa hiyo. Hii ni kutokana na hoja kwamba lugha hizo zinasawiri ujumi, utamaduni, mazingira, falsafa, itikadi pamoja na vipengele vingine vinavyofungamana na ujumi Mweusi. Mtazamo huo unahusishwa na madai ya Nadharia ya Ujumi Mweusi kuwa, matumizi ya lugha ya asili katika kazi ya sanaa ya Kiafrika yanaimarisha ujumi wa jamii na sanaa kwa ujumla (Zirimu, 1971). Matokeo ya utafiti wa makala haya yamebaini kuwa matumizi ya lugha za Kiafrika zenye kusawiri vionjo mbalimbali vinavyosawiri ujumi Mweusi yana mchango mkubwa katika kuonesha kwamba sanaa hiyo inakwenda sambamba na ujumi wa Kiafrika katika maendeleo yake. Lugha kama sehemu ya ujumi wa Kiafrika ina jukumu la kubeba na kuendeleza tamaduni za Kiafrika ndani na nje ya Waafrika wenyewe (Chirambo, 2006). Hali hii inachangia maendeleo ya ujumi katika jamii pana ya Waafrika na dunia kwa ujumla. Mathalani hii inajitokeza katika wimbo *Mimi Mmasai* (2010) wa msanii Mr. Ebbo, msanii anatumia lafudhi ya lugha ya Kimasai katika wimbo huo. Data namba 8 msanii anaimba:
Sipati maziwa nyama kiloviti mmekosa
Nakula maharaki na ugali ngumu kumesa
Saridalama watu nashika faili naishi
Nasema hii masai natembea ushi
Wao nataka mimi faa ndisheti kaoshi
Au masurumbale kama mimi ni tarishi

Data za dondoo namba 8 inadhihirisha kuwa matumizi ya lugha za Kiafrika kwa kuhusisha lafudhi ya lugha ya Kimasai katika wimbo huo. Hali hii si kwa bahati mbaya. Makala imebaini kuwa ujitokezaji wa matumizi ya lugha za Kiafrika katika sanaa wakati mwingine ni kwa ajili ya kueneza lugha za Kiafrika kiulimwengu na pia ni kuwafanya Waafrika kuwa karibu na sanaa yao.

**5.5 Kusisitiza Kuhusu Utu**

Suala la utu katika falsafa ya Waafrika huamini kwamba, utu ni dhana inayotumika kuelezea umuhimu wa mtu kumtendea mwingine sawa na ambavyo angependa naye atendewe. Kwa muktadha huo, mtu ni watu. Utu huhusisha mambo kama kujali, upendo na ukarimu (Mbiti, 2011a). Katika utu huegemea katika 'usisi' badala ya 'umimi'. Hivyo, utu ni kipengele muhimu cha ujumi wa Kiafrika. Kwa Waafrika kila mwanajamii anapaswa kuishi kufuatana na utu (Asante, 1993).

Matokeo ya makala haya yanabainisha kwamba, nyimbo za Bongo Fleva zinasawiri vipengele vya utu kama vile ukarimu, upendo, maadili na vipengele vingine vingi ambavyo vimebainika kuwa na mchango mkubwa katika kuendeleza sanaa hiyo ndani na nje ya Tanzania na Afrika kwa ujumla. Mathalani, katika wimbo *Ndani ya Mateso* (2003) wa msanii Happiness Thadei (p.h.k. Sister P) akimshirikisha msanii Focus na

Thomas. Msanii anaonesha hali ngumu ya maisha inayowakumba watoto yatima jambo ambalo linawafanya watoto hao kukata tamaa. Ingawa hali iko hivyo, msanii anaonesha hali ya utu pale anapomtia moyo yatima. Katika dondoo namba 9 msanii anaimba.

Usijali vitisho yatima
Pole pole yatima pole
Mungu yuko nawe ee!
Usijali vitisho yatima
Una anayekupenda yatima pole
Zaidi, yupo Mungu aliyekuumba

Katika data za dondoo namba 9, msanii anajaribu kumpa faraja mtoto yatima anayepitia mateso na kipindi kigumu. Mbali na hayo, anajaribu kumtia moyo na kumpa ujasiri kwamba Mungu aliyekuumba atamhudumia. Hali hii ni hali ya kuwa na utu na ukarimu kwa wenzetu mara wanapokuwa katika matatizo.Ukarimu ni miongoni mwa tabia inayosisitizwa na kuendelezwa kwa Waafrika (Zirimu, 1971). Akisisitiza kuhusu ukarimu katika jamii za Kiafrika, Yonazi (2019) anaeleza namna Bibiharusi katika jamii ya Waasu (miongoni mwa jamii zinazopatikana nchini Tanzania) huimbiwa nyimbo zinazosisitiza ukarimu siku ya harusi. Na kwamba, anahimizwa kuwa asipokuwa mkarimu nyumba yake itakimbiwa na watu. Kwa maana kwamba jamii haitashirikiana naye katika mambo mbalimbali. Hali hii inadhihirisha kwamba, suala la ukarimu ni kipengele muhimu katika jamii za Kiafrika. Na pia kinasawiriwa katika kazi za kifasihi za jamii ya Watanzania. Mtazamo huo unashabihiana na mawazo ya kinadharia ya Nadharia ya Ujumi Mweusi kwamba tabia ya ukarimu husisitiza wakati wote miongoni mwa jamii za Kiafrika (Taylor, 2010). Aidha, ukarimu huchukuliwa kama miongoni mwa amali muhimu za kijamii, hivyo hurithishwa kizazi hadi kizazi. Kwa muktadha huo, nyimbo za Bongo Fleva zenye kusawiri kwa mawanda mapana suala la ukarimu, hupendwa na huwa endelevu katika jamii ya Tanzania. Jambo hili linachangia kwa kiasi kikubwa nyimbo za Bongo Fleva kuzidi kustawi na kuongeza wigo kimawanda kila uchao.

## 6. HITIMISHO

Makala haya yamechunguza ujitokezaji wa ujumi wa Kiafrika na athari yake katika ushairi wa Kiswahili wa Bongo Fleva. Utafiti huu ulifanyika kwa sababu tafiti kuhusu vipengele vya ujumi wa Kiafrika katika kazi za fasihi zimeishia katika kubainisha ujitokezaji wake hasa katika upande wa maudhui pasi na kuchambua athari yake katika utanzu husika (rej. Laswai, 2015; Omari, 2018; Renatus, 2018; Sanga, A. 2018; Sanga, T 2018 na Elihaki, 2023) hali ambayo inachochea kushindwa kuupa ujumi wa Kiafrika nafasi katika kujenga ama kubomoa kazi husika. Nadharia ya Ujumi Mweusi imeongoza makala haya kubaini vipengele vya ujumi wa Kiafrika katika matini husika. Hii ni kutokana na sababu kwamba, elementi na misingi ya nadharia hii zinaeleza kuhusu ujumi wa Kiafrika moja kwa moja. Pia ni nadharia yenye mwegamo wa kifasihi na kifalsafa hali inayoendana na hali ya makala haya. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, ujitokezaji wa ujumi wa Kiafrika katika sanaa ya Bongo Fleva yana mchango mkubwa katika maendeleo na ustawi wa utanzu wa Bongo Fleva. Vipengele vya ujumi wa Kiafrika kama vile umoja na ushirikiano, ushababi, matumizi ya mazingira asilia ya Kiafrika, matumizi ya lugha za Kiafrika pamoja na utu na ukarimu hayajitokezi tu katika maudhui bali yana mchango mkubwa wa kujenga utalii miongoni mwa nchi na nchi na hukuza diplomasia nzuri baina ya mataifa ya Kiafrika.Aidha, pamoja na hayo husaidia kuteka hadhira pana ya muziki huo Kiafrika, kueneza lugha za Kiafrika huko ulimwenguni pamoja na kujenga umoja wa kisanaa kwa wasanii wa mataifa mbalimbali Afrika na kwingineko. Hivyo, matumizi ya ujumi wa Kiafrika katika sanaa ya Bongo Fleva kumechangia kwa kiwango kikubwa sanaa hiyo kukua, kustawi na kuongeza wigo kimawanda kwa kasi zaidi ukilinganisha na tanzu na vipera vingine vya ushairi wa Kiswahili.

## MAREJELEO


- Armstrong, W.H. (Mh) (1879) *Aesthetics*. London: Bradburg, Agrew $ Co. Printers.
- Ary, D. na Wenzake (2010). *Introduction to Research in Education.* (Toleo 8) Wordsworth: Cengege Learning.
- Asante, K.W. (1993) *The African Aesthetics: Keeper of the Traditions*: ABC-CLO: Incorporate.
- Avidan, L. J. (2023) *Bongo Flava: The Confuence of Popular Music and Politics in Tanzania*.Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha California, California.
- Badru, Z.A. (2015) *Taswira ya Ubainishaji wa Mabadiliko ya Kiujumi katika Vitendawili: Mfano wa Vitendawili vya Kiswahili*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.
- Barret, M.S. (2002) “Towards a Situated View of the Aesthetics in Music Education”. *Journal of Aesthetic Education,* Bloomington Ltd. Juz. Na. 36:123-134.
- Bosanquet, B. (1966) *A History of Aesthetics*. New York: George Allen and Uniwin Limited, New York.
- Bowman, W. (1998) *Philosophical Perspectives on Music*. Oxford University Press. New York.
- Chachage, C.S. (2002) “Ndani ya Bongo: Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni”, Paper
- Chirambo, R. (2006) *Aesthetics and Poetic of Afrocentrcity: Towards a Theory of African Literary Criticism*. Cambrige University Press, Cambrige
- Davier, S. na Wenzake (2009) *A Companion to Aesthetics*.New York: Blackwell Publishing, New York.
- Dorsey, D. (1973) “Black aesthetics” katika *Zirimu, P. na Gurr, A*. East African Literary Bureau, Nairobi.
- Ekwuru, G. (2000) *Towards an African Ethno-Aesthetic: An Igbo Case Study*. Lagos, Longman 300-326

- Elihaki, Y. (2023) "Mabadiliko ya Ujumi Mweusi katika Nyimbo za Muziki wa Dansi 1990-2000". *East African Journal of Swahili Studies*. Juz. Na. 6:89-93
- Fannon, F. (1952) *Black Skin, White Masks*. Edition du Senil, Paris.
- Hume, D. (1975) "Of the Standard of Taste" in *Essay of Moral, Political and Literary*. Oxford University Press, Oxford.
- Ismail, J.H. (2011) "Nafasi ya Nyimbo za Bongo Fleva katika Uelimishaji wa Haki katika Jamii" katika *Mulika*. Juz.29/30: 29-37.
- Jim, P. (2021) *African Aesthetics and The Everday: Community, Healing and Living*. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Lancashire, Cameroon.
- Kant, I. (1960) *Observation on the Feeling of the Beautiful and Sublime,* University of Calfonia Press, Calfonia.
- Kasiga, G. (2023) "Tathmini ya Nyimbo za Muziki wa Kizazi Kipya katika Karne ya 21 Nchini Tanzania. Tija na Madhara Yake". *Mulika* Na. 42 (1)66-82
- Laswai, A. (2015) *Ujumi katika Muziki wa Dansi: Nyimbo Teule za Marijani na Ally Choki*.Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.
- Lopes, A.M. (2015) "Aesthetic Theories" Western Sydney University. https//www.researchgate.net/publication/283348334. Tarehe 30/8/2025.
- Madumula, J. S. (2009), *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Mture Educational Published Limited, Dar es Salaam.
- Mandembwe, C.J. (2011) *Nafasi ya Kejeli na Dhihaka katika Fasihi ya Kiafrika: Mifano Kutoka Tamthiliya Teule za Kimajaribio*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mbiti, J.S (2011a) African Religion and Philosophy. East Africa Education Publishers Ltd, Kampala.
- Mulokozi, M.M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*, Dar es Salaam Kautu, Dar es Salaam.
- Mwanjoka, G. (2011) *Harakati za Bongo Fleva na Mapinduzi*. Dodoma H.M. Dodoma.
- Ojo-Ade, F. (2004) *Being Black Being Human: More Essays on Black Culture Trenton New Jersey*: African World Press.
- Omari, S. (2009) *Tanzanian Hip hop Poetry as Popular Literature*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Omari, S. (2011) "Call Me Top in Dar: The Role of Pseudonyms in Bongo Fleva Music" *Swahili Forum*, Juz.Na 18, 66-69
- Omari, S. (2018) "Ujumi Mweusi katika Kazi za Nathari za M.M. Mulokozi"katika Omari, O. na Samwel, M. (wah) *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 83-110.
- Perullo, A. (2005) "Hooligans and Heroes: Youth Identity and Hip hop in Dar es Salaam Tanzania". *African Today*. Juz. 51 (4) 75-101.
- Presented at the Tenth Conference on the Political Environment in Tanzania, 17th -18th September, Dar es Salaam.
- Renatus, R. (2018) *Ujumi wa Kiafrika katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchunguzi wa Tamthiliya Teule*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa).Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Samwel, M. (2012) *Mabadiliko katika Majigambo: Uchunguzi wa Majigambo ya Jadi nay a Bongo Fleva*. Tazmili ya Uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.
- Samwel, M. (2015) "Bongo Fleva Inapotosha Jamii" Je, Ni Dai Jipya katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili? *Kioo cha Lugha* Na. 10:103-121.
- Sanga, A. N. (2018) "Thamani ya Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi Simulizi za Kiswahili". *Mulika* Na. 40:134-150.Sanga, I. (2011) "Mzungu Kichaa and the Figuring of Identity in Bongo Fleva Musics in Tanzania", in *International Review of the Aesthetics and Sociology of Music*, vol.42 No. 1, Croation Musiological Society.
- Sanga, A. N. (2023) *"Mkengeuko wa Ujumi wa Kiafrika katika Hadithi Fupi za Kiswahili kipindi Cha Utandawazi: Mifano ya Hadithi Fupi kutoka magazeti ya Habari Leo, Nipashe na Mwananchi ya Mwaka 2008 Hadi 2014*" Tasnifu ya Uzamivu katika Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.
- Sanga, T. (2018) "Ujumi wa Mtu Mweusi katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Washairi Teule" katika Omari, S. na Samwel, M (wah) *Fasihi, Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika*. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 111-131.
- Senyamanza, C. (2011) *Misingi ya Kazi za Kubuni: Nadharia n, Mbinu na Mifano ya Kibunilizi.* Dar es Salaam Karlijainer Printing Technology, Dar es Salaam.
- Suriano, M. (2006) "Hip hop and Bongo Flavour Muzic, in Contemporary Tanzania Youth Experience, Agency, Aspirations and Contradictions". Paper submitted for the Conference, "Youth and the Global South, Religion, Politics and the Making of Youth in Africa, Asia and Middle East". Dakar, 13-15 October, 2006.
- Taylor, R. (2010) "Black Aesthetic". *Journal Compilation*. Blackwell Publishing Ltd katika ttps//www.academia.edu/846775/.Philosophy-campass-article-Black Aesthetics, Imesomwa 23 Novemba.2023
- Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi*. Vide-Muwa, Nairobi.
- Williady, H. (2013) *Mabadiliko Kutoka U-Aristotle kwenda Ujadi wa Kiafrika: Mifano kutoka*

*Tamthiliya Teule za E. Husein na P.Muhando*.Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.
- Wolfgang, I. (1975), *The Act of Reading: Theory of Aesthetics Response*, John's Hoplirs University Press.
- Yonazi, E. (2019) *Usanaa wa Lugha katika Ujenzi wa Dhima za Nyimbo za Harusi za Waasu*, Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.
- Zirimu, P. (1971) *Black Aesthetics*. East African Literature Bureau, Nairobi.
- Zirimu, P. na Gurr, A. (1973) *Black Aesthetics* Papers from a Colloquium Held at The University of Nairobi, June 1971, East African Literature Bureau, Nairobi.

**Cite This Article:** Costansia Urassa (2026). Ubainishaji wa Vipengele vya Ujumi wa Kiafrika na Athari yake katika Ushairi wa Kiswahili: Uchunguzi wa Ushairi wa Bongo Fleva. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 9*(3), 67-76.